BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Pili – Tarehe 23 Mei, 2016.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mwenyekiti Kamati ya Wenyeviti:

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Wenyeviti kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2016/2017.

II. MASWALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:

32. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Hivi karibuni Jeshi la Polisi limekuwa likikamata watuhumiwa wa matukio mbali mbali ya uhalifu yakiwemo tindikali, miripuko ya mabomu, nyumba kuchomwa moto na uchunguzi na kesi hizo ni mwisho kuishia kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) bila ya wahusika kufikishwa mahakamani.

a) Hatua ya watuhumiwa kutokufikishwa Mahakamani kunaleta picha gani kwa Serikali katika kusimamia misingi ya Utawala Bora pamoja na Utawala wa Sheria.

b) Hatua ya watu kutuhumiwa makosa ya jinai bila ya kupelekwa Mahakamani, Serikali haioni ndio mwanzo kwa wananchi kuanza kuchukua sheria mikononi jambo ambalo ni kinyume na msingi wa Utawala Bora na msingi wa Haki za Binaadamu.

c) Serikali imechukua hatua gani ya kuchunguza sababu ya kutofikishwa kwa watuhumiwa wa matukio hayo Mahakamani ili kufahamu kama polisi walitekeleza wajibu wao kwa mujibu wa Sheria na kama kuna kasoro nyengine ili kuhakikisha Utawala wa Sheria unachukua nafasi yake katika kupambana na uhalifu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ:

12. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa wafanyakazi wa Serikali za Mitaa wanakazi kubwa sana za kufanya usafi, lakini ndio wafanyakazi ambao hawapati stahiki zao kwa wakati wanapokwenda likizo na pesa za "*overtime*". Na kwa kuwa kuna wafanyakazi ambao ni wazee hawajafika umri wa kumaliza kazi na wanafanyakazi katika mitaro kwa muda mrefu wakati wapo vijana ambao wameajiriwa kwa muda.

a) Je, Serikali haioni kuwa kutokuwalipa haki zao wafanyakazi hawa hatuwatendei haki.

b) Kwa nini wazee hao wasibadilishwe wakapewa angalau kazi nyepesi ili kumaliza muda wao na vijana wakaajiriwa kabisa ili kuepusha uhaba wa wafanyakazi katika Mabaraza.

WAZIRI WA HABARI, UTALII, UTAMADUNI NA MICHEZO:

6. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

Sekta ya michezo ni muhimu sana kwa kuwaunganisha vijana na pia michezo ni sehemu ya Ajira kwa vijana.

a) Je, Serikali imepanga vipi kuhakikisha kwamba sekta ya michezo inakua nchini kwa faida ya vijana wetu na nchi kwa ujumla.

b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuondoa migogoro kwa baadhi ya vyama vya michezo ili kuondoa tatizo la kuanguka kwa kiwango cha michezo Zanzibar.

WAZIRI WA ARDHI, MAJI, NISHATI NA MAZINGIRA:

8. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Wananchi wa Jimbo la Chambani bado wana tatizo la maji katika baadhi ya Shehia ukilinganisha na wakati huu tulionao.

Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia kupata maji wananchi wa Wambaa kwa Azani na Tangi la maji Chambani na Mteng'ombe.

WAZIRI WA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI:

2. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kutokana na mvua zinazonyesha mara nyingi hutokea kujaa maji mengi katika bwawa la Mwanakwerekwe Shelimpya, kunasababisha usumbufu mkubwa wa usafiri katika njia hiyo.

Kwa kuwa tatizo hilo limekuwa la muda mrefu na hadi leo linaendelea. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja katika barabara hiyo.

3. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele): - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kwa ujenzi wa barabara ya Kwerekwe – Fuoni, ambayo ujenzi wake unaendelea vizuri. Kwa kuwa ujenzi huo wa barabara umeenda sambamba na ubomowaji wa nyumba ziliopo karibu ya barabara hiyo.

a) Je, Mhe. Waziri, wananchi waliokumbwa na ubomowaji huo wamelipwa fidia.

b) Ni kiasi gani cha fedha kimetumika kwa malipo hayo.

WAZIRI WA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI:

14. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Wananchi wanahitaji kupewa elimu ya kutosha ili wasiharibu mazao ya baharini na pia wasitumie nyavu za kukokota ambazo hazifai kutumika. Pia wapewe mafunzo na wasaidiwe vifaa vya uvuvi wa kisasa pamoja na zana za uokozi katika mabadiliko hayo.

Je Serikali imejipanga vipi kutimiza malengo yake ya kuimarisha sekta ya uvuvi kwa kuzingatia mambo hayo.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwamba Baraza hili lifikirie na kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2016/2017 na Makadirio ya Mapaato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2016/2017.

Mwenyekiti wa Kamati za Wenyeviti:

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Wenyeviti kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2016/2017.

Zanzibar,
23 Mei, 2016.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA